



SWAHILI *AB INITIO* – STANDARD LEVEL – PAPER 1
SOUAHÉLI *AB INITIO* – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1
SUAHILI *AB INITIO* – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1

Monday 15 May 2006 (morning)

Lundi 15 mai 2006 (matin)

Lunes 15 de mayo de 2006 (mañana)

1 h 30 m

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

KIFUNGU A**SHEREHE! SHEREHE! SHEREHE!**

Tarehe: 30 Aprili, 2006

Mahali: Shule yetu ya Kimataifa

Kiingilio: Shilingi 5000 tu (utapewa na sandiwichi na juisi au soda mlangoni)

Shule inaandaa tafrija au sherehe ya jioni kusherehekeea kutimiza miaka 50 tangu ilipoanzishwa.

Katika ratiba kutakuwa na mambo mbalimbali. Wimbo wa kwaya ya shule utafungua sherehe, halafu utafuatiwa na mambo mengine kama vile vyakula vya mataifa na makabila mbalimbali, maonyesho ya michezo ya kuigiza (tamthilia) na bendi na wanamuziki maarufu watakaopiga muziki baada ya saa 3 usiku. Watu wote mnakaribishwa. Wanafunzi wanaombwa wawaalike baba, mama na ndugu pamoja na marafiki zao. Kiingilio kitakuwa kwa tiketi, na kutakuwa na tiketi 750 tu. Wahi kununua tiketi zako kabla ya tarehe 28 Aprili, 2006.

RATIBA		
	SAA	TUKIO
i	1.00 - 1.10	Wimbo utakaoimbwa na Kwaya ya Shule
ii	1.15 - 1.30	Hotuba ya Mwalimu Mkuu
iii	1.30 - 1.45	Hotuba ya Mwakilishi wa Wanafunzi
iv	1.45 - 2.30	Chakula na vinywaji
v	2.30 - 2.45	Mchezo wa kuigiza
vi	2.45 - 3.00	Mchezo wa bahati Nasibu
vii	3.00 - 3.15	Zawadi mbalimbali kutolewa
viii	3.15 - 3.30	Mapumziko mafupi.
ix	3.30 - 5.15	Muziki na shindano la kucheza dansi
x	5.15 - 5.30	Zawadi kwa walioshinda shindano la kucheza dansi
xi	5.30	Mwisho wa Tafrija/Sherehe

ZAWADI! ZAWADI!

Kutakuwa na mchezo wa bahati na sibu (*prize draws*) wakati wa sherehe, na kama una bahati unaweza kupata zawadi ya redio, *walkman*, simu ya mkononi, tiketi ya ndege kwenda nje ya Afrika, n.k.

WAHI KUPATA TIKETI YAKO KATIKA SEHEMU MOJAWAPO YA HIZI ZIFUATAZO: SHULENI KWETU, MADUKA YA KARIBU NA SHULENI KWETU, VITUO VYA MABASI.

KARIBUNI! KARIBUNI! KARIBUNI! KARIBUNI!

KIFUNGU B

NJIA 10 ZA KULALA VIZURI



Kuna njia nyingi za kukuwezesha kulala vizuri sana. Hizi 10 hapo chini ni njia muhimu kama unataka kulala usingizi mzuri bila usumbufu wowote.

1. FUATA RATIBA. Usichelewe kulala siku za wikiendi. Lala na amka saa zilezile kila siku.
2. USILE WALA KUNYWA SANA. Kabla ya kulala usile wala usinywe sana. Ule chakula cha jioni mapema, ikiwezekana saa mbili kabla ya kulala.
3. EPUKA KAFEINI. Usinywe chai, kahawa wala kinywaji chochote chenye kafeini au kinachosisimua mwili. Ni vibaya pia kuvuta sigara. Vyote hivi vinaweza kukukosesha usingizi mzuri.
4. FANYA MAZOEZI. Ratiba yako ya kila siku ya mazoezi inakusaidia kupata usingizi mzuri. Ratiba hiyo isibadilikebadilike.
5. UBARIDI KIDOGO CHUMBAKI. Chumba chako kiwe na ubaridi kidogo. Joto jingi linamfanya mtu asilale vizuri.
6. USILALE MCHANA. Epuka kulalalala mchana. Tabia hii inakupunguzia usingizi wa usiku.
7. CHUMBA KIMYA. Inafaa chumba chako cha kulala kiwe kimya kwa sababu ukimya husaidia mtu kulala bila kuamkaamka. Usifungulie muziki kwa sauti ya juu. Muziki mwororo wa sauti ya chini unaweza kukusaidia pia kulala vizuri.
8. USAFI WA KITANDA. Tandika kitanda chako vizuri kila siku. Usafi wa kitanda unamfanya mtu afurahie kukilalia.
9. KUOGA. Oga kwa maji ya moto kabla tu ya kulala. Kuoga kwa maji ya moto kunakusaidia uburudike na hukupa usingizi mzito.
10. DAWA. Usitumie dawa za usingizi. Muone daktari wako kabla ya kutumia dawa za usingizi.

TUNAKUTAKIA USINGIZI MWEMA NA NDOTO TAMU.

KIFUNGU C**WATOTO WANASEMA NINI KUHUSU LIKIZO?**

Jina langu ni Tarik Mohamed. Ninasoma Shule ya Msingi ya Atlas iliyoko Ubungo, Dar es Salaam. Mimi likizo yangu nitaitumia kwa kusoma tu. Wala sitakwenda sehemu yoyote zaidi ya kukaa na mama. Unajua kwa nini? Likizo iliyopita nilitembea sana na ndiyo maana nikafanya vibaya katika masomo yangu.

Mimi ninawashauri watoto wenzangu watumie likizo hii kwa kusoma na kufundishwa masomo magumu kama vile Kiingereza.



Mimi ninaitwa Vaileti Hilary. Ninasoma Shule ya Msingi ya Mlimani, iliyoko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Unajua nitafanya nini wakati wa likizo? Weweeeeee, nitasoma sana ili niwe na akili kama maprofesa.

Halafu mama amesema likizo hii tutaenda kumsalimia babu na bibi kule mbali, na kuwatemelea ndugu zetu. Lakini ningependa kuendelea kusoma hapa kama mama akikubali. Akikataa basi tutaenda huko kijijini kwa babu na bibi.

Ninaitwa Amina Shija na ninasoma shule moja na Tarik. Mimi likizo hii nitaitumia kwa kusoma tu wala sitafanya kitu kingine chochote. Unajua kwa nini? Kwa sababu nitakuwa na muda mwangi wa kujifunza masomo magumu na kumwomba kaka anisaidie nisome vizuri.

Mama ameniambia nikiweza kusoma vizuri atanipeleka kuwatemelea marafiki zangu.

Ninaitwa Amani Asei. Ninasoma Shule ya Msingi ya Makumbusho, mjini Dar es Salaam. Mimi likizo hii nitaitumia kwa kuchenza sana. Nitacheza kwa sababu wakati wa masomo sipati muda wa kuchenza mpira wa miguu na watoto wenzangu.

Lakini nitacheza kwa kujificha kwa sababu mama akiniona atanichapa. Mama anasema mtoto mzuri ni yule anayependa kusoma sana.

Mimi ni Kevin Bulele. Ninasoma Shule ya Msingi ya Atlas, hapa Dar es Salaam. Likizo hii nitakwenda kuwasalimia ndugu zangu kwanza, halafu nitaenda kanisani tu. Nikimaliza nitakaa nyumbani na kuanza kusoma kama dada halafu nikisoma vizuri nitakuwa mtu mkubwa mwenye kazi nzuri na pesa nyingi pia.

KIFUNGU D

KARIBU CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM



Chuo Kikuu cha Dar es Salaam! Mahali pazuri sana pa kusomea. Chuo kiko katika mlima kwa hiyo ukiwa Chuoni unaweza kuliona jiji lote la Dar es Salaam na Bahari ya Hindi!

Chuo hiki kina zaidi ya miaka arobaini. Mandhari yake ni nzuri sana. Kuna ghorofa ndefu za mabweni ya wanafunzi, kafeteria tatu kubwa, hoteli au migahawa ya bei mbalimbali:

za juu, za kati na za chini kabisa. Pia kuna maduka makubwa na madogo yenye vitu vya bei za chini, za kati na pia za juu.

Chuoni humo pia kuna misitu na miti mingi yenye wanyama wengi kama vile tumbili na kima, na ndege wa aina mbalimbali wanaoimba nyimbo nzuri mitini. Unaweza kutembea katikati ya misitu hii na kuvuta hewa safi sana yenye harufu nzuri ya maua mengi, hewa ambayo huilipii; au unaweza tu kukaa na kustarehe katika bustani mbalimbali humo chuoni.

Kwa wanaopenda michezo kuna bwawa la kuogelea na viwanja vya michezo kama vile mpira wa miguu, mpira wa vikapu, mpira wa vinyoya, tenisi, voleboli, na kadhalika. Michezo yote haina malipo – ni bure!!!!

Usafiri wa kuja na kutoka chuoni ni rahisi sana hasa kwa mabasi ya daladala, mabasi yaliyojazana katika jiji la Dar es Salaam ambayo nauli yake si ya juu.

Karibu sana na Chuo kuna sehemu mbalimbali ambazo unaweza kwenda kununua vitu mbalimbali au hata kuona filamu.

Karibu sana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambako utajisikia uko nyumbani kabisa japo uko mbali na nyumbani. Kuhusu masomo unayoweza kuyasoma hapo chuoni tafadhali andika barua pepe kwa Afisa Mkuu Taaluma kwa anuani ya taaluma@utawala.chuokikuudar.ac.tz.